

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS**

Anwani ya Simu: **"TUME"**  
DAR ES SALAAM  
Namba ya Simu:0738166703  
Fax: 255 - 022 – 246011  
Barua pepe:  
[secretary@psc.go.tz](mailto:secretary@psc.go.tz)  
Tovuti: [www.psc.go.tz](http://www.psc.go.tz)



TUME YA UTUMISHI WA UMMA,  
6 MTA A WA ALBERT LUTHULI,  
KITALU NAMBA 10,  
S.L.P. 9143,  
**DAR ES SALAAM.**

**WATUMISHI WA UMMA WATAKIWA KUFANYA KAZI KWA  
WELEDI NA NIDHAMU**

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Umma, Jaji (mstaafu) mheshimiwa Dkt. Steven James Bwana amesema wananchi wanahitaji kuona wafanyakazi katika Serikali wanafanya kazi kwa weledi, nidhamu na maadili ya hali ya juu kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa ili kutoa huduma bora na kuharakisha maendeleo yanayotarajiwa na wananchi.

Mheshimiwa Jaji (mstaafu) Dkt. Bwana ameyasema hayo wakati wa kufungua mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume ya Utumishi wa Umma uliofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, na kusema kuwa Tume ni chombo kilichopewa jukumu la kusimamia Rasilimali watu katika utumishi wa umma, hivyo kila mmoja kwa nafasi yake anapaswa kutambua wajibu wake katika kuleta mafanikio ya Tume.

“Baraza la Wafanyakazi na Menejimenti ya Tume wanapopanga Mipango na Mikakati kwa pamoja, hujenga umiliki wa pamoja wa Mipango na ushirikiano katika kutekeleza malengo ya Taasisi. Kwa pamoja mnapata nafasi ya kujipima ni kwa kiasi gani mnafanikiwa, mnapata nafasi pia ya kujadili na kuzitafutia ufumbuzi changamoto zinazowakabili katika kutimiza malengo yenu” alisema.

Akifafanua zaidi alisema, lengo la kuwa na Baraza la Wafanyakazi kama hitaji la kisheria ni kutoa fursa kwa watumishi kupitia wawakilishi wao, kujadili juu ya masuala mbalimbali ya msingi yanayohusu tija na ufanisi kwa upande mmoja na maslahi ya ustawi wao kama watumishi wa umma kwa upande mwingine. Mabaraza

ya Wafanyakazi sehemu za kazi husaidia kuimarisha ushiriki wa kweli wa Wafanyakazi katika kutekeleza majukumu ya Taasisi.

“Baraza la Wafanyakazi lina majukumu yake, nafahamu katika majukumu hayo ni pamoja na kujadili na kushauri kuhusu mipango ya Tume, kupitia na kuridhia makisio ya mapato na matumizi ya Tume. Hivyo, katika Baraza hili mnayo fursa ya kujadili na kutafakari, si maslahi yenu tu bali pia utendaji wenu wa kazi wa kila siku na jinsi ya kuuboresha zaidi” alisema Mheshimiwa Bwana.

Alisisitiza kuwa Serikali imeonesha juhudi kubwa za kuhakikisha watumishi wa umma nchini wanafanya kazi kwa weledi na nidhamu kwa lengo la kufikisha huduma bora kwa wananchi wote.

“Naamini Baraza hili kwa kushirikiana na Tume mtatekeleza kazi muhimu sana ya kusimamia Watumishi wa umma, Waajiri, Mamlaka za Ajira na Mamlaka za Nidhamu kwa kuhakikisha Sheria, Kanuni na Taratibu zote za Umma zinazingatiwa” alisema.

Kwa upande wake, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma, Bw. Nyakimura Muhoji alisema Tume kwa kushirikiana na Baraza imefanikiwa kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na ukaguzi wa kawaida na maalum kwa baadhi ya Wizara, Idara na Wakala ambapo matokeo ya ukaguzi yalisaidia kuongeza uwajibikaji, kuboresha Sera, Sheria na Kanuni kwa Waajiri na watumishi. Watumishi na Watendaji wa umma wamepata elimu kuhusu utekelezaji wa Sheria katika masuala ya Rasilimali watu katika utumishi wa Umma.

“Katika Baraza hili la Wafanyakazi wa Tume ya Utumishi wa Umma, pia tutapitia na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2019/2020 na mwelekeo wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021” alisema Bw. Muhoji.

Imeandaliwa na:

**Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**  
**TUME YA UTUMISHI WA UMMA**  
**16 MACHI, 2020**